

Je, zipo sheria zinazolinda watu wenye ulemavu hapa Tanzania?

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ndiyo, zipo sheria hapa Tanzania zinazolinda watu wenye ulemavu. Tanzania ilitia saina na kuridhia mkataba wa kimataifa wa ulinzi, haki na usawa kwa watu wenye ulemavu mwaka 2006. Kwa kitendo hicho cha kuridhia mkataba huo wa kimataifa Tanzania imeonyesha nia yake ya kuwalinda na kudumisha haki za watu wenye ulemavu. Hata katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 19772 inakataza ubaguzi wa aina yoyote kwa watu wenye ulemavu. Zipo sheria nyingi zinazolinda haki na usawa kwa watu wenye ulemavu ambazo zinahusika na sekta mbalimbali. Kwa mfano; elimu na mafunzo, ajira³, matunzo⁴ na ustawi⁵ kwa ujumla. Ipo pia sera ya Taifa kuhusu ulemavu ya mwaka 20046. Sera hii imeweka mazingira muafaka kwa watu wenye ulemavu kupata haki sawa katika maendeleo ya kijamii, ikiwa ni pamoja na kupata huduma na mahitaji ya msingi kutoka katika jamii.

Sheria zinazolinda haki za Albino

Serikali pia imechukua hatua za kudhibiti hali hii isiendele kutokea ikiwa ni pamoja na kuanza kuwaandikisha rasmi (kufanya sensa) watu wenye ualbino, na pia kuanzishwa kwa ulinzi kwa Albino kupitia jeshi la polisi na jamii kwa ujumla, kwa mfano; watoto Albino wanapokwenda shule. Suala la Albino limeendelea kupewa umuhimu mkubwa kitaifa, ikiwa ni pamoja na mjadala wa kitaifa. Mfano; ujumbe wa mbio za Mwenge wa Uhuru wa mwaka 2009 ulilenga kuhamasisha jamii kuhusu mauaji na vitendo vya kikatili dhidi ya Albino. Mauaji na vitendo vya kikatili dhidi ya Albino vinavyotokea sasa hivi pia vimepelekea serikali kuchukua hatua na kuongeza ulinzi ili kulinda haki za Albino kwa mfano; zimeundwa mahakama maalumu za kusikiliza makosa hayo ili kuharakisha upatikanaji wa haki kwa wahusika. Mpaka sasa watuhumiwa saba wa mauaji ya Albino wamekutwa na hatia na kuhukumiwa kifo kwa kunyongwa.